

# BODI YA KOROSHO TANZANIA



## TAARIFA KWA UMMA KUHUSU MWONGOZO NA.1 WA USIMAMIZI WA MASOKO NA MAUZO YA KOROSHO GHAFI KWA MSIMU WA MWAKA 2019/2020

### 1. UTANGULIZI.

Bodi ya korosho Tanzania (CBT) tayari imeanza usimamizi wa msimu wa Masoko na Mauzo ya korosho ya mwaka 2020/2021 baada ya kutangazwa kuanza kwa msimu wa ununuzi wa korosho tarehe 01 Septemba, 2020 kwenye Mkutano Mkuu wa Wadau wa Tania ya Korosho nchini.

Tarehe 10 Septemba, 2020 Bodi ya Korosho Tanzania ilitoa Mwongozo Na.1 wa Usimamizi wa Masoko na Mauzo ya Korosho Ghafi kwa Msimu wa Mwaka 2020/2021. Mwongozo huo pamoja na mambo mengine unaelezea utaratibu wa uendeshaji wa minada na wadau wote wanaohusika katika hatua zote za ununuzi wa korosho ghafi.

Kufuatia maoni ya Wadau na maelekezo ya Wizara ya Kilimo, Bodi ya Korosho Tanzania imefanya maboresho kwenye utaratibu wa uendeshaji wa minada pamoja na usafirishaji wa korosho ndani ya nchi ili kuongeza ufanisi katika usimamizi wa msimu. Mabadiliko hayo ni kama ilivyooneshwa kwenye sehemu Na.2.0.

### 2. MABORESHO YA VIPENGELE VYA MWONGOZO NA.1 WA USIMAMIZI WA MASOKO NA MAUZO YA KOROSHO GHAFI KWA MSIMU WA 2020/2021

	MWONGOZO NA.1 ULIVYOKUWA AWALI	MABORESHO YA MWONGOZO NA.1 UTAKAVYOKUWA SASA
1	<b>SEHEMU YA NNE</b>	
	<i>Kipengele Namba 4.2.6 Uendeshaji wa Minada kupitia masanduku ya zabuni</i>	
	Kila mnunuzi atatakiwa kuwasilisha na kusajili zabuni yake iliyofungwa kwa lakiri (Seal) kwenye sanduku la zabuni lililopo eneo la mnada kwa kuzingatia eneo linaloweza kufikika kwa urahisi miongoni mwa wakulima, wanunuzi na	Kila mnunuzi atatakiwa kuwasilisha na kusajili zabuni yake iliyofungwa kwa lakiri (Seal) kwenye sanduku la zabuni lililopo eneo la mnada kwa kuzingatia eneo linaloweza kufikika kwa urahisi miongoni mwa wakulima,

	wadau wengine. Zabuni zitapokelewa kupitia sanduku la zabuni kuanzia saa 3.00 asubuhi hadi saa 8.00 mchana na baadae kufunguliwa saa 10.00 alasiri baada ya mauzo kwa njia ya kielektroniki. Sanduku litafunguliwa siku hiyo na mwenye bei ya juu kutangazwa katika eneo la mnada, mbele ya wakulima.	wanunuzi na wadau wengine. Zabuni zitapokelewa kupitia sanduku la zabuni kuanzia saa 3.00 asubuhi hadi saa 10.00 alasiri baada ya hapo sanduku litafunguliwa siku hiyo na mwenye bei ya juu kutangazwa katika eneo la mnada, mbele ya wakulima
2	<b>SEHEMU YA NNE</b> <b><i>Kipengele Namba 4.3.5 Uendeshaji wa Minada kupitia soko la bidhaa</i></b>	
	Mauzo yatafanyika kwa njia ya kielektroniki kuanzia saa 8.30 mchana hadi saa 10.00 alasiri, ambapo wanunuzi watatakiwa kushiriki kwenye mnada kwa kushindana ndani ya muda uliowekwa na bei ya juu itakayopatikana itasubiri ridhio la wakulima ( wastani wa dakika 30)	Mauzo yatafanyika kwa njia ya kielektroniki kuanzia saa 3.00 asubuhi hadi saa 10.00 alasiri sambamba na minada kupitia sanduku, ambapo wanunuzi watatakiwa kushiriki kwenye mnada kwa kushindana ndani ya muda uliowekwa na bei ya juu itakayopatikana itasubiri ridhio la wakulima
3	<b>SEHEMU YA SITA</b> <b><i>Kipengele Namba 6.1.2 Usafirishaji wa korosho ndani ya nchi</i></b>	
	Korosho zitasafirishwa ndani ya nchi kwa kutumia kibali cha kusafirishia Korosho ndani ya Nchi (PDN) inayotolewa na Bodi ya Korosho kwa Njia ya kielektroniki	Korosho zitasafirishwa ndani ya nchi kwa kutumia kibali cha kusafirishia Korosho ndani ya Nchi (PDN) inayotolewa na Bodi ya Korosho kwa Njia ya kielektroniki ambayo itakuwa hai (Valid) ndani ya siku tatu (3),yaani masaa Sabini na Mbili (72), kwa mzigo kufika eneo husika (Destination). Iwapo kutatokea changamoto kabla ya kufikisha mzigo, mnunuzi atatakiwa kutoa taarifa ya maandishi Bodi ya Korosho Tanzania ili kupata kibali kingine.

Pamoja na marekebisho haya, Mwongozo Na.1 wa Usimamizi wa Masoko na Mauzo ya Korosho Ghafi Kwa Msimu wa 2020/2021 unapatikana kwenye Tovuti ya Bodi ya Korosho Tanzania [www.cashew.go.tz](http://www.cashew.go.tz).

Imetolewa na.



Francis Alfred

**KAIMU MKURUGENZI MKUU 22 SEPTEMBER, 2020**